HATUA YA 3: JINSI YA KUMUONGOZA MTU KWA KRISTO

Uamzi wa kumfuata Yesu ni uamzi wa muhimu zaidi katika maisha. Sasa unayo nafasi ya kumwongoza mtu kwa kristo. Muulize swali la uamzi: "Je, ungelipenda kumpokea Yesu maishani mwako?" Kama jibu ni ndio, fanya ombi fupi na muombe yeye akufuatilizie muombe kwa pamoja kwa moyo wake wote na amkaribishe yesu katika maisha yake. Pumzika katika kila neno ili kumruhusu arudie maneno yale kwa ufasaha.

OMBI

"Bwana Yesu, naamini wewe ni mwana wa Mungu. Naamini kwamba ulikufa kwa ajili ya dhambi zangu. Naomba unisamehe dhambi zangu na uje maishani mwangu. Naamini ulifufuka katika wafu na leo u hai. Nakupokea wewe kama bwana na mwokozi wangu. Nitakufuata siku zote za maisha yangu. Amina."

ELEZA VITU MUHIMU KATIKA MAISHA YA UKRISTU:

- **Maombi:** Zungumza na Mungu na ku-jenga mahusiano na yesu.
- **Biblia:** Kusoma neno la Mungu ili uweze kuelewa mapenzi yake, tabia zake na mpango wake.
- **Ushirika:** Tafuta kanisa au ushirika ulio karibu na wewe.
- **Kueneza Injili:** Shirikisha injili na uzoefu wako mpya na Mungu kwa wengine.

Baada ya hapo badilishana mawasiliano na anuani na mkutane pamoja ndani ya siku tatu zijazo. Muombee huyo mtu na mfanye kuwa rafiki. Ikiwezekana, mchukue huyo mtu mkaabudu kanisani, au kwenye kikundi kidogo mkiwa pamoja.

Swahili – Africa

SIKU YA UINJILISITI DUNIANI

Kwa muongozo wa kijitabu cha mafundisho ya HATUA-3 Chenye kurasa- 20 tembelea: www.globaloutreachday.com

MWENDELEZO WA INJILI YA MUNGU - UINJILISITI NI MWENENDO WA MAISHA

Fanya maamuzi ya kushiriki Injili kila mwezi, wiki, au siku na uwe sehemu ya Mwendelezo wa injili ya MUNGU. Kujisajili tembelea: www.god-movement.com

EVERYONE CAN REACH SOMEONE, TOGETHER WE CAN REACH THE WORLD.

Shirikisha shuhuda zako katika mitandao ya kijamii ukitumia alama: **#GlobalOutreachDay**

WERNER NACHTIGAL
Raisi wa Kimataifa
Siku ya Uinjilisiti Duniani

HATUA 3 mini

KATIKA UINJILISTI WA MTU BINAFSI

SIKU YA UINJILISTI DUNIANI

Maono ya Siku ya Uinjilisti Duniani ni kwa kila muumini kushiriki Injili katika siku ya Jumamosi ya mwisho ya mwezi mei kila mwaka. Unaweza ungana na mamilioni ya waumini kutoka ulimwenguni kote ili kushiriki Habari Njema. **Kuwa sehemu hiyo!**

Tembelea tovuti yetu kwa mawazo ya jinsi ya kushirikisha Injili na kushiriki katika Siku ya Uinjilisti Duniani ukiwa na marafiki zako na kanisa.

HATUA-3 ZA MWONGOZO

Mafundisho haya rahisi ya mwongozo yatakupa kile unacho-hitaji kumzungumzia Yesu kwa uhuru na ufasaha. Utajifunza jinsi ya kuwaleta watu kwa Yesu na wao kuwa mashahidi wa kweli kwa aajili yake.

- **Hatua 1: Jinsi ya kuanza mazungumzo**
- **Hatua 2: Jinsi ya kushiriki Injili**
- **Hatua 3: Jinsi ya kumwongoza mtu kwa kristo**

GLOBAL OUTREACH DAY
It's my mission!

HATUA YA 1: JINSI YA KUANZA MAZUNGUMZO

Awali ya yote,ni muhimu kupata umakini wa mtu. Wakati mwanamke msamaria alipokuja kuteka maji, Yesu akamwambia, "Nipe maji ninywe?"(Yohana4:7)

Yesu hakuanza moja kwa moja na mafundisho, ila kwa mada ya siku. Maji yalikuwa ni kiunganishi cha mawasiliano kati yake na Yule mwanamke. Anza mazungumzo yako na "salamu"(Hallo), onyesha tabasamu na urafiki.Pata umakini wake, sikiliza vizuri na tafuta vitu mnavyoshabihiana.

- Anza mazungumzo na kitu cha kawaida cha maisha ya kila siku.
- Uliza swali zuri, kama vile "Je, ulishasikia ya kwamba Mungu anakupenda?"

Ili kuwasiliana kiufasaha,unatakiwa Yule mtu akuamini. Uliza maswali ya wazi, kama vile: "Je,unafikiri nini kuhusu Mungu? "au" hali yako unaendeleje?"

HAMASA

Mara ukishapata mwelekeo wake sisimua Hamasa yake kama ilivyo katika yohana 4:10, Yesu akajibu, "kama ungeliijua karama ya Mungu, naye ni nani akuambiaye, nipe maji…"

Ili umfanye aendelee kuhamasika, chagua mada, kama:

- Nimepata tumaini lililo tofauti katika maisha yangu. Je, Unatafuta tumaini pia?
- Utakuwa wapi ikiwa utakufa leo?

Lakini unaweza usifanikiwe kupata utashi wake kwa kuzungumza tu. Onyesha mwelekeo wa kweli, na watu wengine wataguswa.

MATAKWA

Angalia mtu unayezungumza naye mahitaji yake halisi hasa ni yapi, uyahusishe katika mazungumzo yako. Yesu akamwambia Yule mwanamke: "Nenda, kamwite mumeo uje naye hapa." "Yule mwanamke akajibu akasema, sina mume." Yesu akamwambia, "Umesema vema, sina mume "(yohana 4: 16-18).

Yesu alizungumzia mada halisi iliyogusa maisha halisi ya yule mama, naye akaguswa kabisa. Labda mtu unayezungumza naye hana uhakika na maisha ya milele au kuona ana hatia yoyote. Pengine unaye ongea naye analo tatizo au ni mgonjwa. Yesu alikutana na watu katika mahitaji yao. Mungu bado anaponya wagonjwa, kurejesha ndoa, na kuwaweka watu huru kutoka katika vifungo. Hata hivo tatizo kubwa ambalo kila mtu analo ni kujitenga mbali na Mungu.

KISA CHAKO

Kisa chako binafsi ni muhimu sana! Elezea kisa chako kwa namna ya kusisimua. Usitumie maneno ambayo mtu mwingine hata yaelewa, na usiongezee maneno. Kisa chako kiwe katika sehemu tatu:

- Maisha yako yalifananaje hapo kabla?
- Ilikuwaje hadi ukapata kumjua Yesu?
- Nini kimebadilika katika maisha yako?

Jaribu kuona ni vitu gani vimekupa kusudi katika maisha au ni kwa jinsi gani Mungu alikubadilisha. Kisa chako kiwe tofauti. Elezea kisa chako katika njia ambayo hata wana-okusikiliza watajilinganisha.

HATUA YA 2: JINSI YA KUSHIRIKISHA INJILI

Injili inaweza tu kuokoa mtu kama ataelewa na kuamini. Unaweza ielezea injili katika namna nne zifuatazo.

MPANGO WA MUNGU

Ulikuwa ni mpango wa Mungu tangu mwanzo kufanya urafiki na mwanadamu. Hapo mwanzo kila kitu kiliumbwa kwa ukamilifu. Kulikuwa hakuna vita, hakuna dhuruma, hakuna magonjwa,---kila kitu kilikuwa timilifu na kamili. **Mwanadamu aliishi kwa amani na utulivu na Mungu.**

Mungu akaona kila kitu alichokifanya na tazama ni chema sana – Mwanzo 1:31

TATIZO

Mwanadamu akaamua kumwacha Mungu na kufata njia zake mwenyewe. Leo tunaweza kuona matokeo ya maamuzi ya Mwanadamu badala ya kuendelea kuishi kwa amani na utulivu kati yao tunaona sasa uongo, chuki, wivu, magonjwa na vita kila mahali.
Hata hivyo, mbaya zaidi ni kutengana na Mungu milele. Tatizo ni kwamba, katika juhudi zetu binafsi hatuwezi kupatana na Mungu. Madhehebu mbalimbali yana-jaribu kwa kila njia kuwa karibu na Mungu tena. Kwa sababu ya dhambi, tumetengwa mbali na Mungu.

Hakuna mwenye haki hata mmoja – Warumi 3:10

UPENDO WA MUNGU

Mungu ni wa kweli na hawezi kudharau dhambi. Kwa kuwa Mungu anatupenda, alikuja na mpango madhubuti wa ku-muokoa kila mmoja, hii ina maana kuwa unaweza kurudishwa katika mahusiano mazuri na yeye.
Mungu alionyesha upendo wake wa kweli kwa kumtuma mwanawe wa pe-kee, yesu kristo, katika ulimwengu huu ili afe msalabani kwa ajili ya kila mtu.
Kwa kufanya hivyo, Yesu alibeba adhabu kwa ajili ya dhambi zetu. Na siku ya tatu, Yesu akafufuka toka katika wafu, kama alivyosema atafufuka. Na leo hii anaishi, na katika yeye, njia ya kwenda kwa Mungu imefunguliwa.

Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulim-wengu, hata akamtoa mwanawe pekee ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. – Yohana 3:16

UAMUZI WAKO NI UPI?

Matendo yetu mema, juhudi zetu, kuvuta hisia na kuhudhuria kanisani havitoshi kufika kwa Mungu. Kuna njia moja tu: **Tu-natakiwa kumgeukia Yesu na kujitenga mbali na hali ya maisha tunayoishi sisi wenyewe.**

Kwa sababu, ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa , "Yesu ni Bwana" na kuamini kwa moyo wako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. – Warumi 10:9